

Unachohitaji Kujua kuhusu Huduma za Afya za Elektroniki kwenye Kliniki ya Afya Shuleni

Je, Ziara ya Huduma za Afya za Elektroniki kwenye SBHC ni nini?

Ziara ya huduma za afya za elektroniki kwenye Kituo cha Afya Shuleni (School-Based Health Center, SBHC) inaweza kufanyika wakati unaenda kumwona mtoa huduma wako kwenye kliniki iliyo katika mojawapo ya shule za APS. Ukiwa hapo, kliniki hutumia kompyuta kuunganisha kwa watoa huduma kwenye eneo jingine la SBHC lililo Albuquerque. Mtoa huduma anaweza kuunganishwa kwa kiungo cha video ya moja kwa moja na sauti. Njia nyingine ya ziara ya huduma za afya za elektroniki ni wakati uko nyumbani na uunganishwe kwa mtoa huduma wa SBHC kwa kutumia kompyuta au kifaa cha elektroniki. Njia hii hukuruhusu kufikia watoa huduma ili kukusaidia bila kuhitajika kusafiri hadi walipo.

Je, faragha yangu inalindwa vipi?

- Faragha yako inalindwa kama tu ziara ya ana kwa ana
- Kile ambacho wewe na watoa huduma mnasema na kuona katika ziara za video ya moja kwa moja hutendeka kwenye mfumo maalum wa kompyuta salama. Hii inamaanisha kuwa hakuna mtu mwingine anayeweza kuona wala kusikia kinachotendeka.
- Tutafanya kila tuwezalo kuifanya ziara na matokeo yako kuwa ya faragha
- Ziara ya huduma za afya za elektroniki hazirekodiwi

Je, hatari zinazoweza kutokea ni zipi?

- Huenda kukawa na matatizo kwenye muunganisho wa kompyuta. Hiyo inamaanisha kuwa huenda watoa huduma za afya shuleni wasiweze kujifunza mambo muhimu. Au huenda ziara ikaratibiwa upya.
- Tunakuwa waangalifu sana ili kulinda ziara za huduma za afya za elektroniki. Lakini inawezekana usalama wetu ukawa na tatizo. Jambo hili likitendeka, kuna uwezekano wa taarifa zako za afya kutosalia za faragha.

Je, Haki Zangu ni Zipi kuhusu Ziara za Huduma za Afya za Elektroniki?

- Unaweza kusimamisha ziara wakati wowote. Unahitaji tu kusema unataka kusimamisha.
- Si lazima uwe na ziara zaidi za huduma za afya za elektroniki ikiwa hutaki, hata kama daktari wako anafikiria kuwa litakuwa jambo zuri.
- Una haki ya kuambiwa kumhusu kila mmoja aliye katika chumba chako katika kliniki ya SBHC wakati wa ziara za video za moja kwa moja. Pia una haki ya kujua kuhusu mtu yeyote anayehitaji kuja kwenye chumba. Kwa mfano, ikiwa kuna tatizo kwenye kompyuta, fundi anaweza kuhitaji kuja ili kulitaua. Unaweza kuondoka kwenye chumba ukitaka hadi mtu huyo aende. Pia unaweza kumwomba mtu huyo aondoke ukitaka.
- Una haki ya kupata nakala ya rekodi zako za matibabu. Unaweza kupata nakala kwa kufuata hatua za kawaida kwenye kliniki yako.
- Wewe au bima yako inaweza kutozwa na UNM Medical Group SBHC kwa ziara. Uliza kwenye mapokezi maswali yoyote kuhusu bili ambayo unadaiwa.